HOTUBA YA SPIKA WA BUNGE MHE. SAMUEL J. SITTA (MB) KWENYE UZINDUZI WA MFUKO WA VYOMBO VYA HABARI TANZANIA, KARIMJEE TAREHE 3 DESEMBA, 2008

Mhe. Sophia Simba (Mb),
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora);

Bi. Elieshi Lema;
Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya Mfuko;

Bw. Ernest Sungura,
Mratibu wa Mfuko wa Vyombo vya Habari;

Bw. Reginald Mengi,
Mwenyekiti wa MOAT;

Bw. Ayoub Rioba,
Mwenyekiti wa MISA – Tanzania;

Wafadhili wa Mfuko;

Waheshimiwa Mabalozi;

Wawakilishi wa Vyama vya Wanahabari;

Ndugu Wanahabari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana:

Mwaka jana Mwanahabari wa Ulaya aliyebobea Winters Negbenebor, katika makala yake yenye kichwa cha habari **Globalization, Independent Media and Development in Africa**: **Theatre of the strong and the mighty:** aliandika yafuatayo kuhusu Vyombo vya

Habari katika Bara la Afrika, nanukuu: ***"At this point, it is very evident that Africa needs nothing more than a better and more democratic media system for its growth and development. Only an African press genuinely committed to the freedom of the media, respect for human rights, respect for people's welfare and development can bridge the gap and sail Africa to the much desired promised land. A Better Media. A Better Africa."***

Maneno haya yanatukumbusha ukweli mzito kwamba kwa kwetu Afrika taaluma ya uanahabari haina budi kuzingatia safari yetu ndefu na ngumu ya kuleta maendeleo ya kweli kwa watu wetu. Kwa hiyo, naushukuru uongozi wa Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania kwa kunialika kujumuika nanyi katika tukio hili muhimu kwa nchi yetu la kuzindua Mfuko wa Vyombo vya Habari. Nawashukuru pia kwa heshima mliyonipa ya kuwa Mgeni Rasmi kwenye hafla ya uzinduzi wa Mfuko huo ambao una lengo la kuimarisha Sekta muhimu ya Habari hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Sekta ya Habari hapa nchini imekua kwa kasi katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Nimearifiwa kuwa hivi sasa kuna vituo vya redio 45 kote nchini, vituo vya televisheni 27 na magazeti 60. Hata kijijini kwangu Urambo tuna vituo viwili vya "*Cable television!"* Bado hapo hujahesabu *blogs* kama vile *Jamii Forums, Michuzi blog* nk. Kupanuka huko kwa Sekta ya Habari kunaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache

za Afrika zenye kiwango cha juu cha ukuaji wa Sekta ya Habari. Kwa baadhi yetu ambao ni wasomaji makini wa magazeti, hivi sasa, ukipenda kufanya hivyo unahitaji zaidi ya saa tatu kuyapitia magazeti yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Katika hafla hii nimeona vema nizungumze nanyi masuala manne yafuatayo: -

- Sekta ya habari na Maendeleo ya Nchi;
- Uandishi bora wa habari na unaozingatia maslahi ya nchi;
- Serikali na Vyombo vya Habari;
- Changamoto mbalimbali.

Sekta ya Habari na Maendeleo ya Nchi:

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Sekta ya Habari ina mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi – hususan nchi maskini kama Tanzania. Mbali na kuelimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali, Vyombo vya Habari husaidia kufichua vitendo vinavyokwamisha maendeleo ya nchi kama vile ufisadi, rushwa katika utawala, matumizi mabaya ya madaraka, huduma mbovu kwa wananchi, ubadhirifu wa mali ya umma nk. Tunayo mifano mingi katika nchi yetu ambapo Vyombo vya Habari kwa ujasiri na bila woga vimekuwa mstari wa mbele katika kufichua maovu. Nawapongeza kwa dhati kutokana na mchango wenu wanahabari wa

kupambana na maovu nchini kwa ujasiri mkubwa. Aidha, Vyombo vya Habari pia huchangia kuwepo uwazi na uwajibikaji *(transparency and accountability)* katika utawala ambavyo ni msingi muhimu wa utawala bora. Ni dhahiri kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya maendeleo ya nchi na uimara wa Sekta ya Habari katika nchi husika. Nchi nyingi maskini hususan katika Bara letu la Afrika zina mifumo na sheria ambayo inagandamiza uhuru wa Vyombo vya Habari. Kwa mfano hapa kwetu Tanzania kwa yeyote mwenye mtazamo chanya atabaini kwamba Sheria ya Magazeti (1976) imepitwa na wakati. Natoa wito kwa Serikali kuharakisha kufikisha Bungeni Muswada wa Sheria mpya ya Habari itakayolingana na hali ya sasa. Nachukua fursa hii kuupongeza uongozi wa Mfuko wa Vyombo vya Habari kwa kubuni wazo la kuanzisha Chombo hiki. Aidha, Nawashukuru wahisani kwa kujitolea kugharamia Mfuko huu kwa kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo.

Uandishi bora wa Habari na unaozingatia Maslahi ya Nchi:

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Kila nchi ina maslahi yake *(national interests)* ambayo hufafanuliwa kwenye Sera ya Mambo ya Nje ya nchi husika. Ni maslahi haya ambayo huitofautisha nchi au jamii moja na nchi nyingine. Ni kwa msingi huo, Tanzania ya Nyerere ilijengwa katika misingi inayozingatia usawa, udugu, uadilifu, kuwajali wanyonge na kutowabagua watu kwa misingi ya rangi ya mtu, dini yake, kabila lake, eneo analotoka au jinsia yake. Ni misingi hii ambayo imetufanya tuendelee kuwepo kama

Taifa moja lenye umoja na mshikamamo katika kipindi cha miaka 47 ya Uhuru wetu. Ni misingi hii ambayo imejenga taswira ya Watanzania kuwa ni watu waungwana, wamoja na wenye utamaduni wa ushirikiano na ukarimu. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwepo vitendo, kauli, mitazamo ya baadhi yetu kuashiria mwekekeo wenye nia ya kuibomoa misingi hii kupitia kwenye Vyombo vya Habari. Vyombo vya Habari ni mojawapo ya nyenzo inayotumiwa na watu hawa. Si kazi ngumu kuvitambua vyombo hivi vichache vya Habari kwani vinajidhihirisha waziwazi kwa kuandika habari za uchonganishi, uzushi na kueneza hisia za chuki na utabaka. Mfano mmoja wa habari za uchonganishi ni pale ambapo mwandishi anapotosha hoja au taarifa kwa makusudi na anaamua kujenga hoja juu ya msingi huo alioupotosha!

Hii ni tabia moja mbovu mbovu ambayo hutumiwa na waandishi wasio waadilifu kwa lengo la upotoshaji yaani kupotosha nukuu ama unavyomnukuu kiongozi na kisha kujenga hoja juu ya upotoshaji ulioufanya mwenyewe. Kwa mfano, Agosti mwaka huu nilipotamka kule Bungeni kwamba mizania ya haki za binadamu hapa nchini imeegemea kuwalinda zaidi wahujumu uchumi wakubwa, mwandishi wa gazeti moja lenye mwelekeo wa kutetea mafisadi alipotosha kuwa mimi ni mwanasheria nisiyejali haki za binadamu. Nilichosema ni kwamba, haki za binadamu za mtu mmoja mmoja ambaye kwa vitendo vyake anahujumu mamilioni haziwezi kutazamwa bila kuzingatia haki za hao mamilioni. Ni wajibu wa nchi yoyote na hasa nchi maskini kuangalia kuwa haki za binadamu hazitoi mwanya: - (1) Kujenga tabaka la watu maalum ambao utaratibu wa

kuwashughulikia unakuwa tofauti na watu wengine (2) Wala rushwa wakubwa wanaohujumu uchumi wa Taifa kujisikia wana uhuru mpana wa kuendeleza maovu yao huku hali ya wengi ikididimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Hali hii isipodhibitiwa mapema itauvunja umoja na utengamano wetu na kutuingiza kwenye migawanyiko, machafuko na hatimaye hata vita vya wenyewe kwa wenyewe. Hatuna budi kuviimarisha Vyombo vya Habari makini vyenye nia njema na nchi yetu dhidi ya vichache vinavyotumiwa na waovu. Kwahiyo, nimefurahi kusikia kuwa, lengo la Mfuko huu ni kuvijengea uwezo Vyombo vya Habari na wanahabari ili kuandika na kutangaza habari za kina, za ukweli, zilizofanyiwa utafiti na zinazoweka mbele maslahi ya nchi. Kwa maneno mengine, Mfuko huu unaanzishwa ili kuijenga taaluma ya Habari katika misingi ya uadilifu, kujali taaluma na ukweli. Nawashukuru na kuwapongeza wote waliofanikisha kuasisiwa kwa Mfuko huu ambao ni dhahiri utaipandisha juu zaidi fani ya Habari nchini.

Ushirikiano baina ya Vyombo vya Habari na Bunge:

Vyombo vya Habari hujulikana kama Mhimili wa Nne wa Dola *(Fourth State).* Kama nilivyotangulia kusema hapo awali, kazi kuu ya Vyombo vya Habari ni kuelimisha, kuhabarisha, kuburudisha, kufichua maovu, kuhamasisha nk. Ili kutekeleza kazi hii kwa ufanisi, Vyombo vya

Habari havina budi kushirikiana kwa karibu na Asasi na Taasisi nyingine za utetezi wa Wananchi hususan Asasi za Kiraia na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Dk. Essop Pahad – aliyekuwa Waziri katika Ofisi ya Rais huko Afrika ya Kusini mnamo mwaka 2006 aliwahi kusema yafuatayo kuhusu uhusiano kati ya Bunge na Vyombo vya Habari: ***"...it must be accepted that parliament without media is as barren a scene as media without parliament. The two Institutions, Parliament and Media though independent in any democracy, are complementary in their activities and effects. Neither can do without the other, they are in this sense collaborators in the same cause – the cause of enlightment and good governance of citizens. The relationship of these two Institutions with one another, and their interaction with those other great Institution found in any democracy, the executive and judiciary are crucial to the cause of good governance!! "***

Mhe. Mwenyekiti na Wageni Waalikwa,

Kama mnavyofahamu, Bunge ni Chombo cha Uwakilishi wa wananchi. Hivyo, kwa maneno mengine Waheshimiwa Wabunge ambao kwa sasa idadi yao ni 323 wanawakilisha sauti, mahitaji na matarajio ya sisi Watanzania wote milioni arobaini. Wananchi kwa upande wao hawana budi kupata taarifa ya namna wawakilishi wao

wanavyotekeleza majukumu yao kwa niaba yao. Hii hi haki yao ya msingi. Ni kupitia Vyombo vya Habari ambapo Wananchi hupata taarifa za namna Wabunge wanavyotekeleza majukumu yao na hivyo kupima ikiwa ajenda za wananchi zinazingatiwa Bungeni. Aidha, Vyombo vya Habari pia ni nyenzo muhimu katika kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge kuisimamia na kuishauri Serikali. Kwa kutumia taarifa na makala mbalimbali za Vyombo vya Habari, Waheshimiwa Wabunge hupata taarifa na takwimu mbalimbali ambazo huzitumia kuiuliza Serikali maswali, kuchangia wakati wa mijadala ya Bajeti na ya Miswada ya Sheria. Ni ukweli uliojidhihirisha siku za hivi karibuni kuwa ajenda na hoja nzito zinazojadiliwa Bungeni ama huibuliwa kwanza na Vyombo vya Habari, au huendelezwa na kufafanuliwa na vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Hivyo, ni wazi kuwa bila Vyombo vya Habari, Bunge haliwezi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kama nilivyotamka hapo awali, vyombo hivi viwili vinategemeana. Kutokana na kutegemeana huko hivi sasa Ofisi yangu katika Mpango Mkakati wake wa miaka mitano (2008 – 2012), imeweka moja ya vipaumbele vya Mpango huo kuwa ni kuinua ubora wa Uandishi wa Habari za Bunge. Katika mpango huu, programu za mafunzo ndani na nje ya nchi zimeandaliwa ili kuwajengea uwezo waandishi wa Habari za Bunge. Tayari Ofisi yangu iliwasiliana na Wahariri wa Vyombo vya Habari na wametuletea majina ya waandishi ambao watakuwa mahsusi kwa ajili ya uandishi wa habari za Bunge. Naamini kuwa Mfuko tunaouanzisha

hii leo utaunga mkono jitihada za Ofisi yangu ili kuipa nguvu dhana hii ya ushirikiano baina ya wanahabari na Bunge.

Serikali na Vyombo vya Habari:

Katika suala la mahusiano baina ya Serikali na Vyombo vya Habari, hali ni tofauti kidogo. Kumekuwepo mivutano baina ya Serikalli na Vyombo vya Habari. Mivutano kama hii ipo pia katika nchi nyingi nyingine hata zilizoendelea. Mivutano hii inatokana na haja ya wanahabari au Vyombo vya Habari kufichua mambo ya hovyo yanayofanywa na Serikali na Serikali kutokuwa tayari kuruhusu mambo yake kuanikwa kwa umma. Naiona hali hii kuwa inakinzana (*paradoxical*).

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Nasema hivyo kwa kuwa Serikali inatazamiwa kutekeleza kazi zake kwa nia njema kabisa ya kuwaletea Wananchi maendeleo. Hivyo, Wananchi wanayo haki ya kupata taarifa ya namna Serikali inavyoshughulikia kero zao na matatizo yao. Ni kweli kuna masuala ambayo kwa umuhimu wake hususan yale yanayohusu usalama wa nchi hayawezi kuwekwa wazi kwa kila mtu. Hata hivyo, siafiki kuwa hata mikataba ya masuala ya uchumi au biashara ambayo Serikali imesaini kwa ajili ya kuisaidia nchi na wananchi wake pia iwe ni siri. Kuna mantiki gani kwa Waziri anayeenda ughaibuni kutuambia kuwa anaenda kuingia Mkataba wenye maslahi yetu wananchi na baadaye akirejea atuambie kuwa walichokubaliana ni siri kwetu na hata kwa wawakilishi wetu yaani – Bunge! Tutapimaje basi ikiwa maslahi ya

nchi yamezingatiwa au mhusika kaenda **"kuiuza"** nchi! Nawakumbusha Wizara zote makubaliano yetu na Serikali kwamba wanao wajibu wa kumpatia Katibu wa Bunge mikataba yote ya maendeleo ambayo sasa imetengewa masjala mahsusi kwa ajili ya kuwapa nafasi Wabunge waiangalie. Wanaoendeleza dhana ya usiri dhidi ya mwenyemali (mwananchi) wanalo jambo! Wasakamwe ili waache mizengwe hiyo.

Tukumbuke ni usiri huo huo ambao huwalazimisha wanahabari kuandika habari za kuhisi au kile wanachokiamini kuwa ni sahihi. Nadhani katika mazingira haya wa kulaumiwa si mwandishi bali Serikali. Hivyo, nashauri wenzetu Serikalini kuweka utaratibu ulio wazi wa kila Wizara kuwa na deski la taarifa ambapo wanahabari na wananchi wanaweza kupata habari za uhakika kuhusu utekelezaji wa majukumu yaliyo chini ya Wizara husika.

Changamoto:

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Naomba nimalizie hotuba yangu kwa kuainisha changamoto chache zinazoikabilli Sekta ya Habari Tanzania.

☎🗁◑Ongezeko la Vyombo vya Habari lisiloendana na idadi ya wanataaluma waliobobea kwenye fani ya uandishi wa habari;

☎🗎◑Vyombo vingi kushabikia habari za kisiasa zaidi kuliko habari zinazohusu matatizo ya msingi ya kijamii kama UKIMWI, umaskini, mazingira nk;

☎🗎◑Vyombo vingi vya habari kujielekeza kwenye habari na matukio ya maeneo ya mijini na kuyasahau maeneo ya vijijini ambapo Watanzania wengi ndiko waliko;

☎🗐◑Umuhimu wa kufuatilia mienendo ya Idara za Serikali zenye mifumo mibovu na utendaji kazi uliojaa urasimu, usumbufu na huduma duni kwa wananchi.

Watendaji wengi wanafanya kazi zao kwa mazoea tu. Vyombo vya Habari vitusaidie kumulika uozo huo kwa sababu Watanzania tunastahili huduma bora zaidi kutoka kwa Serikali yetu kuliko ilivyo sasa. Na wakati wote mbaki katika ukweli. Msiyumbishwe. Waovu wote wafichuliwe. Msije mkatufikisha pahala ambapo katika nchi moja ya Afrika alisikika mwananchi aliyekata tamaa akisema: ***"It is a strange thing to live in my country! 90% of what you are told are lies but the lies are more familiar than the truth so it is the truth that seems unbelievable!"***

Naamini kuwa Mfuko wa Habari Tanzania tunaouzindua leo utajielekeza katika kukabiliana na changamoto hizo ili hatimaye kukidhi kiu ya habari miongoni mwa Watanzania.

Hitimisho:

Mnamo mwaka 2005 Wakfu wa Shirika la Utangazaji la BBC *(BBC World Service Trust)* ulituma mapendekezo matano kwenye Tume iliyoundwa na Waziri Mkuu Mstaafu wa Uingereza Tonny Blair kuhusu Afrika *(Commission for Africa).* Mapendekezo haya yalihusu mchango wa Vyombo vya Habari kama kichocheo cha maendeleo barani Africa. *The role of media as an agent of change in Africa).* Katika pendekezo lake la pili, Wakfu ulipendekeza kuundwa kwa Mfuko wa Vyombo vya Habari vya Afrika *(Create an African Media Development Fund).* Pendekezo hilo linasema hivi, nanukuu: ***"The full potential of African media to advance its own development will not be realized without a significant increase in assistance to help strengthen, train and reform existing media. While numerous and respected efforts to train journalists exist, the overall picture is fragmented and under-resourced, leading to an African media which is below global standards and unable to help drive the continent's development goals. Additionally, the prevalence of state-owned media, and lack of demand for reform, is a significant barrier to seeing the benefits media can bring to communities."***

Mfuko tunaouzindua leo unakidhi haja ya kuimarisha Sekta ya Habari Tanzania kwa maendeleo ya watu wake. Nawashukuru sana wadau wa Mfuko huu kwa kuona umuhimu wa kuwa na Chombo hiki na kujitolea kwa wahisani kuuwezesha katika kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo.

Kwa mara nyingine tena naushukuru uongozi wa Mfuko wa Habari Tanzania kwa mwaliko wenu ulioniwezesha kukutana na hadhara hii jioni ya leo. Nawatakia mafanikio katika azma yenu hii njema.

Sasa natamka kuwa Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania umezinduliwa rasmi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.